**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA - TABORA**

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA**

**DR.BATILDA BURIAN**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SERIKALI TANZANIA

**SEKONDARI YA WASICHANA DR.BATILDA BURIAN**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA**

**MKOA WA TABORA**

**MEI 2024**

**TABORA**

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS – TAMISEMI

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA ,**
**DR.BATILDA BURIAN,**
**S.L.P 56,**
**KALIUA-TABORA.**
**10/05/2024**

**Namba za Simu:**

**Mkuu wa Shule:0756020660**

**MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI ……….............**
**JINA LA MWANAFUNZI:……………………………………………...**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA DR.BATILDA BURIAN HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA MKOA WATABORA MWAKA 2024/2025 .**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024/2025 na atasoma tahasusi ya …………...

Shule ya Sekondari ya **DR.BATILDA BURIAN** ni shule ya vipaji ya watoto wa kike, ipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua, Kata ya Igagala, katika kijiji cha Wachawaseme kilichopo Igagala namba tisa (9), umbali wa Kilometa thelathini na nane (38) kutoka kituo cha treni cha Kaliua ,na umbali wa kilometa thelathini na sita (36) kutoka kituo kikubwa cha mabasi cha Kaliua, Kusini mwa Mji mdogo wa Kaliua.Shule imepakana na barabara kuu ya lami inayotoka mji mdogo wa Kaliua kuelekea mkoa wa Kigoma. Kutoka stesheni au kituo cha mabasi unaweza kutumia usafiri wa mabasi makubwa/Coaster

zinazokwenda Kigoma au Noah / Coaster zinazokwenda Usinge/Isawima na utashuka kijiji cha Wachawaseme - Igagala namba tisa (9) au kwa msaada omba ushushwe sekondari mpya ya vipaji ya wasichana.Usafiri wa basi kutoka mjini Kaliua unapatikana katika kituo kikubwa cha mabasi Kaliua, Nauli ni Shilingi elfu tatu hadi elfu nne (3,000/= , 4,000/=) .Hakuna usafiri wa bajaji wala pikipiki kwani gharama ni kubwa sana.
Muhula wa Masomo unaanza tarehe............................ hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe.......................... Mwisho wa kuripoti ni tarehe …………………………..

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za darasani**

i. Sketi ya shule ni draft (angalia sampuli ya kitambaa kwenye fomu hii) kwa maelezo ya mshono **NI RINDA BOX (MBELE NA NYUMA) IWE NA MARINDA MATATU KULIA NA MATATU KUSHOTO**, urefu ifike kwenye kifundo cha miguu.
ii. Aje na mashati 02 meupe yenye mikono mifupi yenye ukosi wa kuvalia tai kwa wakristo;
iii. Waislamu waje na kanzu fupi (short kanzu) nyeupe 02,urefu wake ni hadi kwenye hipsi .Rangi ya juba ni nyeupe kwa darasani na nyeusi kwa kushindia ,ifunike kifua cha mwanafunzi,pia iwe na mikono mirefu inayofika mwanzo mwa kiganja akisimama.
iv. Nguo za kuvaa ndani ya shati ambazo ni sidiria /vest za rangi nyeupe au nyeusi .Haturuhusu uvaaji wa nguo zenye rangi tofauti na hizi.
v. Tai fupi /neck tie rangi ya sketi, ziwe mbili (angalia mchoro kwenye fomu hii)
vi. T-shirt ya shule nzito rangi moja ya kijivu aina ya manga.
vii. Soksi ndefu zinazofika kwenye magoti rangi ya kijivu zenye mistari miwili ya bluu na nyeupe katikati sehemu ya juu, jozi mbili,na soksi nyeusi jozi moja tu.
viii. Sweta 01 la rangi ya kijivu lililofumwa kwa uzi mzito wa kufumia
ix. Viatu ya shule jozi mbili rangi nyeusi ,vinavyofungwa kwa kamba na viwe na visigino vifupi,lakini visiwe na muundo wa buti

**2.2 Sale za michezo**

i. Raba nyeupe jozi moja
ii. soksi nyeupe ndefu zinazofika kwenye magoti(stocking),jozi mbili


iii. T-shirt ya pink mpauko yenye kola ya duara,isiwe na maandishi wala michoro ya rangi yoyote ile.
iv. Tight fupi nyeusi kwa ajili ya kuvalia ndani ya sketi ya michezo
v. Sketi ya pink mpauko, kitambaa cha kunguru, mshono wa solo ya kuzunguka yenye ufito mweupe chini na mikanda kwa ajili ya kufunga.
vi. Nguo za kuvaa ndani za kutosha.


**2.3 Sare za kushindia**

i. Shamba dress gauni mbili kitambaa kizito cha suti rangi ya dark maloon (zingatia sio maloon) kwa ajili ya kushindia ,urefu ni kufunika kifundo cha minguu kwa dini zote, kwa wenye mahitaji maalumu (wenye ualbino) shamba dress iwe na mikono mirefu.
ii. Tracksuit rangi ya kijivu jozi moja,yenye mistari myeupe pembeni (ambayo atavaa wakati wa kujisomea usiku)
iii. Viatu vya wazi(open shoes) kwa ajili ya kushindia jozi mmoja.

**AINA YA VITAMBAA VYA SARE**

I.KITAMBAA CHA SKETI YA DARASANI II.KITAMBAA CHA SKETI YA MICHEZO






III.GAUNI LA KUSHINDIA NI KITAMBAA AINA YA TR NAMBA MOJA DARK MALOON (ZINGATIA SIO MALOON)

# MISHONO WA SARE ZA SHULE

1. SKETI YA DARASANI (DRAFT)



2.





3. SHAMBA DRESS (GAUNI LA KUSHINDIA) - MBELE




SHAMBA DRESS - NYUMA



4. TIE



**2.4 Vifaa vya darasani.**

i. Madaftari 09 (counter Book quire four 4);
ii. Madaftari 06 (counter Book quire 2);
iii. Vitabu vya masomo vya tahasusi husika (vitabu vilivyochapishwa na TIE);
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific calculator;
vi. Boksi la kalamu za wino, na penseli boksi moja aina ya 2HB
vii. Mkebe wa vifaa vya Hisabati(Mathematical set)
viii. Ream papers A4 (02) – Zikabidhiwe shuleni
ix. Boksi file (file kubwa) – 01

**2.5 Vifaa vya usafi**

i. Ndoo tupu ndogo (lita 10) zenye mifuniko ambazo hazijatumika - 02
ii. Fyekeo - 01,
iii. Jembe na mpini wake viwe vipya - 01,
iv. Reki - 01,
v. Mfagio wa kufagilia ndani (softibloom) wenye mpini mrefu - 01
vi. Mifagio imara ya chelewa ya kufagilia nje yenye mpini mrefu - 02
vii. Brashi fupi imara ya kusugulia vigae (tiles)- 01
Viii.Brashi imara ya kusugulia sinki la choo yenye mpini mfupi na kibakuli chake – 01
Ix.Brashi imara ngumu(hard bloom)yenye mpini mrefu ya kusuguria sakafu – 01
x. Kibandizio (squeezer) - 01

**2.6 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:**

i. Picha 4 passport size akiwa amevaa shati la shule (jeupe) na ziwe na kivuli (background) ya bluu nyuma.
ii.Tranka kubwa la kutunzia vifa vyake na kufuri imara kwa ajili ya usalama wa vitu vyake .
iii.Taulo (01),vitenge au kanga doti (01) ambavyo atajifunga Wakati wa kwenda kuoga.
iv. Kandambili/Ndala kwa ajili ya kuogea pea (01)
v. Godoro lenye ukubwa wa 2.5"x6"- 01
vi.Mashuka 02 na foronya 01 vyenye rangi ya pink
vii.Shuka 01 na foronya yake vyenye rangi nyeupe.

viii.Mto (01)
ix.,Blanketi kwa ajili ya kujifunika baridi - 01
x..Chandarua 4"x 6" (*rangi nyeupe ) - 01*
xii.Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko , kikombe na chupa ya chai).
xiii.Dumu la maji ya kunywa la lita 05 – 01
xiv.Cheti cha kuzaliwa (njoo na nakala moja)

**NB:- Ukipata changamoto yoyote ya vifaa piga simu upate maelekezo**.

**2.7 Michango mbalimbali ya shule**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wako wa mwili,kutunza mavazi yako muda wote na kuhakikisha nguo zako zimekunjwa na kuwekwa vizuri kwenye tranka

na kutunza mazingira ya shule,lakini pia kufanya usafi katika maeneo yote ya shule.

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote kulingana na nyakati na mazingira,

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

ix. Kutunza mali za shule ikiwa ni pamoja na kuhakikisha hakuna bomba linalotiririsha maji ovyo,taa za umeme kuzimwa kwa wakati,matumizi sahihi ya vyoo vyote vya shule,na utunzaji wa majengo na samani za shule.

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali kama kisu, panga,fyekeo n.k na ni marufuku kutunza vifaa vya usafi bwenini na dawa bila idhini ya daktari .

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini awapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake, au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika kwa mwanafunzi mmoja tu.**
- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).
- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kuja nyumbani kwa ajili ya msiba wa mama, baba ,mlezi,kaka au dada ( ndugu wa familia moja na mwanafunzi kwa maana wa tumbo moja/baba mmoja tu) na sio ndugu wengine.Taarifa za msiba ziletwe moja kwa moja kwa Mkuu wa shule na sio kwa mwanafunzi.Mwanafunzi hataruhusiwa kuja nyumbani endapo utaratibu huu utakiukwa.**
- ❖ **Ni marufuku kuvaa kandambili (slippers)wakati wa chakula katika bwalo la chakula au mazingira yoyote ndani na nje ya shule ,isipokuwa bafuni tu wakati wa kuoga na bwenini.**
- ❖ **Wageni wa mwanafunzi wanaotambulika shuleni,ni wale walioandikishwa kwenye faili la mwanafunzi,na**

**wanaruhusiwa kumbembelea mwanafunzi mara moja tu kwa muhula(mara mbili kwa mwaka)siku moja kabla ya mahafali ya kidato cha sita muhula wa kwanza na cha nne muhula wa pili kwa kuitwa na uongozi.Wazazi/walezi wasifike shuleni endapo hawajaitwa na uongozi wa shule.**

- **Likizo zote mwanafunzi atakapolazimika kwenda likizo ni sharti arudi nyumbani kwa wazazi /walezi wake ,haruhusiwi kwenda kwa ndugu ( ubalozini) kipindi cha likizo fupi wala ndefu kwa kutokea shuleni moja kwa moja.**

**4. Makosa yanayoweza kusababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha migomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi kama vile kuvunja kiti/meza/mlango/kabati au madirisha ,kupasua vioo n.k
xix. Kuibia mitihani.

**Viambatisho  Muhimu vya Fomu hii:**

i. Fomu Na.I: Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu Na.2:Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu Na.3: Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

## FORM NO. 1

## THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## PRESIDENTS' OFFICE

## REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

## FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

To be completed by a medical Officer in respect of all Form I and Form V entrants.

Pupil's full name…………………………………………………………………………

Age/Years……………………………………Sex………………………………………

Blood found (red and White)…………………………………………………………….

Stool examination:……………………………………………………………………….

Urinalysis:………………………………………………………………………………..

Venereal Diseases test:…………………………………………………………………..

T.B. test:…………………………………………………………………………………

Eye Test:…………………………………………………………………………………

Ears:………………………………………………………………………………………

Chest:…………………………………………………………………………………….

Spleen:……………………………………………………………………………………

Abdomen:………………………………………………………………………………..

Urine for Pregnant:………………………………………………………………………

ADDITIONALL INFORMATION (If any) e.g. Physical defects, impairment(s) e.g. arm, leg etc. infection chronic or family disease etc.

…………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………..

I certify that the above is fit to pursue further education as stated above.

Signature: …………………………….

Designation: ………………………Station: …… ……………Date: …………..……………………...
Official Stamp: ………………………

**FORM NO. 2**

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA DR. BATILDA BURIAN**
**TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

1. JINA LA MWANAFUNZI…………………………………………………..
2. KABILA……………………………………………………………...
3. TAREHE YA KUZALIWA……….MWEZI…………….MWAKA………….
4. AMEZALIWA KATIKA WILAYA YA…………………………………….
   MKOA WA……………………………………………………………..
5. DINI……………………DHEHEBU……………………………………......
6. JINA LA MZAZI/MLEZI……………………………………………………
   (Ikiwa mzazi amefariki andika jina la mlezi hapa)
7. ANWANI YA MZAZI/MLEZI:
8. S.L.P ……………………...
9. KIJIJI/MTAA ………………..
10. TARAFA …………………….
11. WILAYA/KATA …………………
12. MKOA ……………………………

Na. ya simu ya mzazi/mlezi…………………………………………….

13. KAZI YA BABA/MLEZI…………………………………………………….
14. KAZI YA MAMA/MLEZI…………………………………………………………..
15. Afya ya mwanafunzi (kama ana ugonjwa unaohitaji uangalizi uandikwe: Taja udhaifu wowote wa mwili au afya yake na uambatanishe cheti cha Daktari).
    ……………………………………………………………………………….
    ……………………………………………………………………………….
16. Majina ya Ndugu wengine wanaohusika na malezi ya huyu mwanafunzi (matatu tu), anuani zao kamili na Namba zao za simu na picha zao za passport zibandikwe kwenye maboksi mbele ya jina la ndugu.

(a) Ndugu:(Majina matatu) ………………………………………………………...
Uhusiano na Mwanafunzi:……….…………………………………………

Anwani : S.L.P ………………………………………………………………..

Namba ya simu: ……………………………………………………………….

(b) Ndugu:(Majina matatu) ………………………………………………………...
Uhusiano na Mwanafunzi:……….…………………………………………

Anwani : S.L.P ………………………………………………………………..

Namba ya simu…………………………………………………………..

(c) Ndugu:(Majina matatu) ………………………………………………………...
Uhusiano na Mwanafunzi:……….…………………………………………

Anwani : S.L.P ………………………………………………………………..

Namba ya simu: ……………………………………………………………….

**SAINI YA MWANAFUNZI………………….. TAREHE ………………………………**

**FORM NO. 3**

**MKATABA/ AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi…………………………………………. (jina kamili) ambaye ni mwanafunzi, nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa, ninakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na shule hii.

Ninaelewa wazi kwamba shuleni ni mahali pa kujifunza na mimi nina nia ya kujifunza. Ninaelewa pia kuwa nafasi hii niliyopewa ni dhamana, hivyo naahidi mbele ya wazazi/walezi wangu ya kwamba nitaitumia vema nafasi hii kwa kushirikiana na uongozi wa shule kutimiza na kutekeleza yale yote yaliyo katika maagizo haya. Nitatii na kufuata sheria za shule wakati wote. Naahidi kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Naahidi pia kufanya bidii katika masomo yangu na kuwa mfano mwema kwa wenzangu wakati wote.

Jina laMwanafunzi ………………………………………………………….

Saini ya mwanafunzi………………………………………………………….

Tarehe………………………………………………………………………….

Shahidi(Mzazi /Mlezi)

Jina kamili………………………………………………………………………..

Saini……………………………………………………….

Tarehe……………………………………………………….

**N.B:**

**I. Hakikisha mtoto anakuja na kadi ya bima ya afya,kwasababu gharama za matibabu ni kubwa sana na ni gharama ya mzazi.**

**II. Kwa siku za hivi karibuni, kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu, na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.**
**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KUPITIA NAMBA ZILIZOPO KATIKA FOMU HII.**

**III. Fomu hii ina kurasa 12 zenye maandishi,tafadhari njoo na fomu hii ikiwa na kurasa zote 12 ,na fomu ya hospitali ikiwa imejazwa kwa ukamilifu.**

**IV. Tafadhari soma kwa makini maelekezo/maagizo yote katika fomu hii na uyatekeleze kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA YA DR.BATILDA BURIAN**

..............................................

**MWL.AVODIA A.NSHUNJU**

MKUU WA SHULE
SEKONDARI YA WASICHANA
DR.BATILDA BURIAN
S.L.P 56 KALIUA-TBR.